Jina ........................................................................................ Namba yako ....................................

102/2
**KISWAHILI**
Karatasi 2
Julai/Agosti 2014
**Muda: Saa 2½**

Sahihi ya Mtahiniwa ......................................

Tarehe ......................................................

For More Free KCSE Past papers Visit www.freekcsepastpapers.com

# MTIHANI WA TATHMINI YA PAMOJA
# WILAYA YA WESTLANDS

**KISWAHILI**
Karatasi 2
Julai/Agosti 2014
**Muda: Saa 2½**

**MAAGIZO**

a) Andika jina lako na namba yako katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
b) Weka sahihi yako na tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
b) Jibu maswali **yote.**
c) Andika majibu yako yote katika nafasi zilizoachwa katika kijitabu hiki cha maswali.
d) Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| 1 | 15 | |
| 2 | 15 | |
| 3 | 40 | |
| 4 | 10 | |
| Jumla | 80 | |

## 1. UFAHAMU

Rais wa jamhuri ya Kenya, wabunge, viongozi mbalimblai na wananchi, ningalipenda kuchukua wakati huu kuwakaribisha katika hafla hii ya kwanza kukudhuriwa na rais wetu nikitumai nyote ni wazima.

Kenya ni mojawapo ya mataifa ya Afrika yaliyokabiliwa pakubwa na uzorotaji wa usalama. Hii inatokana na ulafi na ubinafsi kutoka kwa viongozi wenye nyadhifa mbalimbali. Tukichukulia kwa mfano, walinda usalama wanapokula mlungula ili mihadarati ipitishwe nchini kutoka nje, huwa na dhamira gani ilhali wanafahamu fika kwamba wengi wa wakora pamoja na wabakaji hutumia dawa hizi ndiposa kufikia upeo huo wa kutekeleza unyama,

Usalama vijijini ni jambo lililochukuliwa kuwa jepesi mathalani ya uyoga kwani si kitu cha kustaajabisha kusikia kuwa adinasi amedungwa kisu hadi kuf, sababu kamili ikiweza kuwa wizi wa yai la kuku . Je, yai la kuku laweza kugharimu maisha ya mja? Hii inatokana na uzembe wa askari wanaolinda usalama vijijini.

Mahakamani jaji anapopewa kitu kidogo ili alalie kesi upande mmoja ili kumkinga ambaye labda ameua, amebaka au labda kuvunja duka la mwenyewe, huwa hasa haki za kibinadamu pamoja na usalama uko wapi kwani pindi tu anapowachiliwa huru mtu huyu , anaweza kuzusha janga kuu lingine kuliko lililopita?

Maafisa wa barabara wanapoona gari limejazwa kupita kiasi, dereva anaendesha gari ilhali hajahitimu au gari bovu lisilostahili kuendeshwa barabarani, halafu wafuate kunyamaza au wazunguke mbuyu, usalama na maisha ya watu huwa yamelinganishwa na nini? Pengine ni kitu kisichokuwa na thamani.

Baadhi ya wananchi wasio wazalendo wanaoshughulikia viriba vyao tu wanaposhirikiana na nchi za ughaibuni kupitisha silaha hatari kama bunduki na zinginezo huwa wanawaza nini? Wanakosa kung'amua kwamba
hivi ndivyo vifaa vitakavyowaua. Yote haya yanatokana na walinda usalama kutowajibika vilivyo. Kwa kweli nchi yetu imeharibika mno hivyo basi ni lazima wazalendo washirikiane usiku na mchana kupambana na ufisadi, ugaidi uliokithiri, unyama na maovu menginéyo yaliyoenea vururu kote nchini.

Serikali ni lazima ijitahidi kuimarisha shughuli zake kote nchini. Hii inamaanisha kwamba, viongozi wawe watu wa kupenda maendeleo. Majaji mahakamani wawe waaminifu, polisi waimarishe usalama barabarani na kuwatoza faini wanaoenda kinyume na sheria.

Wananchi wawe watu wa kutumia bongo zao na kutambua ni nani anayefaa kufuatwa kwani vita vya kikabila ni vya kukera hasa tunaposikia wafuasi wa chama fulani wamepigana na wafuasi wa chama kingine sababu zikiwa ulafi wa wanasiasa.

Wananchi wenzangu tukizingatia haya nchi yetu itakuwa salama na pahali pazuri pa kuishi. Asanteni sana kwa kunipatia muda wenu.

a) Tambua dhamira ya hatibu. (alama 2)

.................................................................................................................................

.................................................................................................................................

b) Taja sababu kuu inayochangia katika kuzorota kwa usalama nchini. (alama 1)

.................................................................................................................................

.................................................................................................................................

c) Thibitisha kuwa maisha ya watu yamekosa thamani. (alama 2)

.................................................................................................................................

.................................................................................................................................

.................................................................................................................................

For More Free KCSE Past papers Visit www.freekcsepastpapers.com

d) Taja na ueleze jinsi makundi mbalimbali yanavyochangia kuzorota kwa usalama. (alama 4)

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

e) Usalama unaweza kuimarishwa nchini. Onyesha ukweli wa kauli hii. (alama 1)

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

f) Dondoa na utoe maana ya tashbishi moja iliyotumiwa katika kifungu. (alama 2)

i) Alalie kesi

..................................................................................................................................

ii) Ughaibuni

..................................................................................................................................

iii) Wanaoshughulikia viriba vyao tu

..................................................................................................................................

For More Free KCSE Past papers Visit www.freekcsepastpapers.com

## 2. UFUPISHO

**Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.**

Uneni "mfumko wa bei" ni uneni wa kibiashara. Mfumko wa bei unaletwa na bidhaa kuwa haba, na hivyo basi, kuwa ghali. Bidhaa zikipungua, huwa kila mtu anazihamu na kuzisaka kwa tunu. Hii hali ya bidhaa yoyote kuwa kitu cha tunu huifanya thamani ya bidhaa hiyo kupanda. Thamani ya bidhaa ikipanda basi bei ya bidhaa hiyo nayo hupanda.

Kwa upande mwingine, bei ya bidhaa ikipanda, huhitajika pesa nyingi kuliko kawaida kuinunulia bidhaa hiyo ambayo thamani yake huwa imepanda pia. Huku kutumia pesa nyingi kununulia bidhaa huifanya thamani ya pesa kushuka. Matukio haya mawili kwa pamoja, yaani kupanda kwa thamani ya vitu na kushuka kwa thamani ya pesa, ndiyo yanayosababisha mfumko wa bei. Mfumko wa bei, hivyo basi, ni hali inayosababishwa na pesa nyingi zisizo na thamani kubwa sokoni ili kununulia bidhaa chache zilizopanda bei ghafla kuliko ilivyo kawaida.

Mfumko wa bei ulimwenguni umesababishwa na maendeleo ya kiteknolojia. Zana za kiteknolojia ni ghali kutengeneza, na ni ghali kutumia. Ni ghali kuzitumia kwa sababu zinahitaji vitomezi kadha wa kadha ili zifanye kazi barabara. Vitomezi hivi havitolewi bure, bali navyo pia hununuliwa. Aidha, zana hizi zinahitaji kufanyiwa marekebisho mara kwa mara. Ili kuzirekebisha vinahitajika vipuri. Hivyo vipuri navyo hunuliwa. Kununua vipuri, zinahitajika fedha, tena nyingi sana kutegemea thamani yake.

Ni wazi basi, kwamba jinsi ulimwengu unavyozidi kuendelea kiteknolojia, bidhaa nyingi zinazohitajika ili kujiendeleza kimaisha zitazidi kutoka viwandani. Kujenga viwanda, na kuvifanya vizalishe bidhaa ni pesa nyingi kutumika. Na bidhaa iliyokamilika kwa kutumika pesa nyingi, yenyewe huwa ghali. Huku kuwa ghali kwa vitu vitokavyo viwandani ndiko kunakofumua bei.

Sasa tukiutazama ulimwengu wa leo, tutakuta ya kwamba nyenzo yake kubwa ni teknolojia. Hata

mkulima katika nchi inayoendelea hawezi kuepukana na umuhimu wa kutumia zana za kisasa za ukulima iwapo anataka kutajirika. Ndipo matajiri ulimwenguni wakazidi kutajirika ilhali maskini nao wanazidi kuwa maskini. Hii ni kwa sababu kuwa tajiri kunahitaji matumizi ya pesa nyingi ili kuweza kuelea katika teknolojia ya kisasa badala ya kuzama. Maskini kama ijulikanavyo hawana hiyo mijipesa ihitajikayo.

Je, mambo yatakuwaje katika karne hii ya 21 itakayokuwa na maendeleo ya kasi kupindukia ? Katika karne hii ya maajabu, ulimwengu huenda ukafikia upeo wake kiteknolojia. Jambo la kwanza, viwanda vitakuwa ni nyenzo iliyopitwa na wakati katika maendeleo ya mwanadamu. Mawasiliano ndiyo yatakayokuwa bidhaa muhimu. Katika muktadha huo, tarakilishi ndicho kitakachokuwa chombo mahususi katika kupitisha habari muhimu za biashara na nyinginezo. Tarakilishi ina vitomezi vyake kama vile programu na vinginevyo. Kwa mtu yeyote kuwa na vitomezi hivi, ni sharti fedha nyingi zitumike kwa sababu vinabadilika mara kwa mara. Wazi ni kwamba mfumko wa bei utaendelea kupanda.

For More Free KCSE Past Papers Visit www.freekcsepastpapers.com

**Maswali**

a) Kwa kurejelea aya nne za kwanza eleza kinachosababisha mfumko wa bei ulimwenguni. (Maneno 65) (alama 7)

Matayarisho

Jibu

b) Fupisha aya za mwisho mbili kwa maneno 75. (alama 8)

Matayarisho

..................................................................................................................................................

..................................................................................................................................................

..................................................................................................................................................

..................................................................................................................................................

..................................................................................................................................................

Jibu

..................................................................................................................................................

..................................................................................................................................................

..................................................................................................................................................

..................................................................................................................................................

..................................................................................................................................................

..................................................................................................................................................

..................................................................................................................................................

..................................................................................................................................................

..................................................................................................................................................

..................................................................................................................................................

For More Free KCSE Past papers Visit www.freekcsepastpapers.com

## 3. MATUMIZI YA LUGHA

i) Andika sentensi ifuatayo katika hali yakinishi : (alama 2)
Wanafunzi wasiposoma kwa bidii hawatapita mtihani

..................................................................................................................................................

..................................................................................................................................................

ii) Andika sentensi ifuatayo kwa udogo. (alama 2)
Mbwa hao watachanjwa kesho kutwa

..................................................................................................................................................

..................................................................................................................................................

iii) Tumia kivumishi kionyeshi kisisitizi cha mbali kidogo na nomino katika ngeli ya KU (alama 2)

..................................................................................................................................................

..................................................................................................................................................

**iv)** Bainisha kiima na chagizo katika sentensi ifuatayo : (alama 2)
Mafahali wale walipigana mchana kutwa

.......................................................................................................................

.......................................................................................................................

**v)** Bainisha yambwa katika sentensi ifuatayo : (alama 3)

Muuguzi alimbebea daktari makasi kwa toroli.

.......................................................................................................................

.......................................................................................................................

.......................................................................................................................

**vi)** Toa mfano wa neno lililo na silabi ya konsonanti. (alama 1)

.......................................................................................................................

**vii)** Ainisha vitenzi katika sentensi ifuatayo :
Mjomba alikuwa akipanda mahindi shambani. (alama 2)

.......................................................................................................................

.......................................................................................................................

.......................................................................................................................

**viii)** Changanua sentensi ifuatayo ukitumia vishale : (alama 4)

Mahabusu alikimbia haraka huku askari akimfuata polepole

.......................................................................................................................

.......................................................................................................................

.......................................................................................................................

.......................................................................................................................

.......................................................................................................................

.......................................................................................................................

**ix)** Tofautisha sauti zifuatazo : (alama 2)
a) / t /

.......................................................................................................................

b) / d /

.......................................................................................................................

For More Free KCSE Past papers Visit www.freekcsepastpapers.com

x) Huku ukitoa mifano mwafaka, onyesha matumizi mawili ya kibanishi katika sarufi. (alama 4)

....................................................................................................

....................................................................................................

....................................................................................................

....................................................................................................

xi) Andika kwa kinyume :
Baba ameingia chumbani mwake (alama 1)

....................................................................................................

....................................................................................................

xii) Tambua mzizi katika neno 'walisaidiwa' (alama 1)

....................................................................................................

xiii) Tambua viambishi awali na tamati katika neno 'kililiwa' (alama 2)

....................................................................................................

....................................................................................................

....................................................................................................

xiv) Andika kwa wingi :
Chumvi ya jirani ilimwangu na kondoo wangu (alama 2)

....................................................................................................

xv) Bainisha vishazi katika sentensi ifuatayo : (alama 2)
Gaidi aliyelipua guruneti ile ametiwa mbaroni.

....................................................................................................

....................................................................................................

....................................................................................................

xvi) Andika viwakilishi ngeli vya nomino zifuatazo : (alama 2)
a) Pahali

....................................................................................................

b) Jongoo

....................................................................................................

xvii) Andika katika msemo wa taarifa :

"Nitakujulisha nikimpata," Saidi alisema. (alama 2)

....................................................................................................

....................................................................................................

For More Free KCSE Past papers Visit www.freekcsepastpapers.com

**xviii)** Tunga sentensi ukitumia neno 'seuze' (alama 2)

..............................................................................................................

**xix)** Bainisha aina za virai katika sentensi ifuatayo : (alama 3)

Sheria hizo mpya zilitundikwa juu ya ukuta usiku wa manane.

..............................................................................................................

..............................................................................................................

..............................................................................................................

For More Free KCSE Past papers Visit www.freekcsepastpapers.com

## 4. ISIMU JAMII

Eleza kwa ufupi jinsi Kiswahili kilivyoenezwa nchini Kenya katika kipindi kabla ya uhuru. (alama 10)

..............................................................................................................

..............................................................................................................

..............................................................................................................

..............................................................................................................

..............................................................................................................

..............................................................................................................

..............................................................................................................

..............................................................................................................

..............................................................................................................

..............................................................................................................

..............................................................................................................